**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu+255262963313/2963314*
*Nukushi: +255 26 296 3316*
*Barua pepe: ps@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Mji wa Serikali Mtumba,*
*S. L. P 2908,*
***40477 DODOMA***

## TAARIFA KWA UMMA

## UTOAJI HUDUMA ZA ARDHI KUPITIA MFUMO WA e-Ardhi

**26 Septemba 2025, Dodoma**

Wizara inaendelea kuboresha utoaji wa huduma za ardhi kupitia mfumo wa ***e-Ardhi*** ambao unalenga kurahisisha utoaji wa huduma kwa kuwawezesha wananchi kupata huduma popote walipo. Mfumo wa e-Ardhi unatumika katika shughuli za upangaji, upimaji, umilikishaji ardhi, usajili na uthamini. Mikoa ya Dodoma, Arusha, Tanga, Mbeya na Mwanza na Halmashauri za Manispaa za Shinyanga, Mtwara Mikindani, Kigoma Ujiji, Mji wa Nzega, Wilaya za Kahama, Chalinze na Songea zimeanza kutumia mfumo huu. Aidha, kwa huduma za uthamini na usajili wa nyaraka za kisheria, mfumo huu unatumika katika mikoa yote nchini.

**Wizara inawaalika wananchi,** t**aasisi za kifedha, mawakili na wadau wengine kujisajili katika mfumo wa e-Ardhi** kupitia http://eardhi.lands.go.tz ili kupata huduma za ardhi kwa urahisi na haraka.

Aidha, Wizara inapenda kuutaarifu umma kuwa utumiaji wa mfumo huu umesababisha mabadiliko ya muonekano wa nyaraka. Hivyo, wananchi wanajulishwa kuwa wanaweza kuthibitisha uhalali wa nyaraka zilizotolewa kupitia mfumo huo kwa *ku-scan* alama maalum (Barcode) zilizowekwa kwenye nyaraka husika.

Kwa maelezo zaidi kuhusu usajili na namna ya kutumia mfumo huu, tembelea tovuti ya Wizara: www.lands.go.tz au piga simu kupitia huduma kwa wateja **Na. 0262161610/0739646885** au wasiliana na Ofisi ya Ardhi iliyopo katika Wilaya na Mkoa wako.

Imetolewa na

**Eleuteri E. Mangi**
**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**